Ubatizo

“Kwa ubatizo tunakiri imani yetu katika kifo na ufufuo wa Yesu Kristo, na kushuhudia kufia kwetu dhambi na kusudi letu la kuenenda katika upya wa uzima. Hivyo tunamtambua Kristo kama Bwana na Mwokozi, tunakuwa watu wake, na tupokelewa kama washiriki na kanisa lake. Ubatizo ni mfano wa muungano wetu na Kristo msamaha wa dhambi zetu, na kumpokea kwetu Roho Mtakatifu. Ni kwa kuzamishwa majini na unategemea uthibitisho wa imani katika Yesu na ushuhuda wa toba ya dhambi. Unafuata mafundisho katika Maandiko Matakatifu na ukubali wa mafundisho yake.” (Rum.6:1-6; Kol.2:12, 13;Mdo.16:30-33; 22:16;
2:38; Mt.28:19, 20))

Nyangwira aliyeishi Afrika ya Kati, hakuona ubatizo kuwa ni jambo la ziada. Kwa zaidi ya mwaka moja alijifunza Biblia. Alitamani awe mkristo. Jioni moja alimwambia mume wake aliyojifunza. Akiwa amehamaki, mume wake alibwatuka, “sitaki dini ya namna hii nyumbani kwangu na ukiendelea kujifunza huko, nitakuua.” Pamoja na kuvunjwa moyo, Nyangwira aliendelea na mafundisho na akawa tayari kubatizwa. Kabla ya kuondoka kwenda kubatizwa, alimwambia mume wake kuwa anaenda kubatizwa. Mume wake alishika upanga, akamwambia, “nilikuambia sitaki ubatizwe, na siku utakayobatizwa, ntakuua.” Hata hivyo Nyangwira alidhamiria kumfuata Bwana na aliondoka kwenda kubatizwa mwangwi wa vitisho vya mume wake vikiwa masikioni mwake. Kabla ya kuingia majini, aliungama dhambi zake, akatoa maisha yake kwa Yesu, pasipo kujua kwamba huenda akawa anautoa na uhai wake pia kwa siku hiyo. Amani ilijaa moyoni mwake alipobatizwa. Aliporudi nyumbani, alichukua upanga wa mume wake akamwendea alipo. Mume wake alipomwona aliuliza kwa hasira, “Je, umebatizwa?” “Ndiyo” Nyangwira alijibu kirahisi akiendelea, “hapa kuna upanga”. Mume akahoji, “Je, uko tayari kuuawa? Mke akajibu“Ndiyo.” Akishangazwa na ujasiri, mume wake hakuwa na nia ya kumwua tena.

Ubatizo una umuhimu gani?
Je, ubatizo una umuhimu hata mtu akahatarisha maisha yake? Je, Mungu anaudai kwa lazima? Je, wokovu wetu unategemea kuwa tumebatizwa au la?

Kielelezo cha Yesu. Siku moja Yesu aliacha karakana ya seremala Nazareti, akaaga familia akaenda Yordani ambako binamu yake Yohana alikuwa akihubiri. Alipomkaribia Yohana, aliomba abatizwe. Kwa mshangao, Yohana aliuliza, mie nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? “Kubali hivi sasa” Yesu alijibu, “kwa kuwa ndivyo itupasayo kuitimiza haki yote.” (Mt.3:13-15). Ubatizo wa Yesu ulifanya desturi hii iwe ya kimbingu. (Mt. 3:17 cf. Mt.21:25). Ikiwa Yesu asiye na dhambi alibatizwa kutimiza haki, sisi wenye dhambi twapaswa nasi kubatizwa.

Amri ya Yesu. Mwishoni mwa huduma yake duniani, Yesu aliagiza “Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu na kuwafundisha yote niliyowaamuru ninyi (Mt.28:19, 20). Yesu alitaka wote wanaouingia ufalme wa neema, wote wanaoutamani ufalme wake wabatizwe na kusisitiza, na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari. (Mt.28:20). Baada ya kupaa, wanafunzi walihubiri umuhimu wa ubatizo (Mdo.2:38; 10:48; 22:16). Kuitikia wito huu, umati wa watu walibatizwa na kuunda kanisa la Agano Jipya, (Mdo.2:41, 47; 8:12) wakikubali mamlaka ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Ubatizo na Wokovu. Yesu alifundisha, aaminiye na kubatizwa ataokoka. (Mk.16:16). Katika kanisa la mitume, ubatizo ulifuata kumwamini Yesu, kuthibitisha imani ya muumini. (cf.Mdo.8:12; 16:30-32). Petro anasema kama Nuhu alivyookolewa kwa safina, sisi tunaokolewa kwa ubatizo (1Pet.3:20, 21). Siyo safina iliyomwokoa Nuhu bali ni Mungu, nasi si maji ya ubatizo yanayotuokoa, bali ni damu ya Yesu. Ila imani yetu inavyoonyeshwa kwa njia ya ubatizo, hutufanya kuupokea wokovu. Pamoja na ubatizo kuhusishwa na wokovu, hautoi uhakikisho wa kuokolewa. Mtume Paulo akitumia kielelezo cha taifa la Israeli, anasema wote walibatizwa katika wingu na katika bahari, wakala chakula na kunywa kinywaji cha roho lakini Mungu hakupendezwa na wengi wao. (1Kor.10:1-5). Ubatizo hautuhakikishii wokovu moja kwa moja na yule adhaniye amesimama, aangalie asianguke. (1Kor.10:11, 12)

Ubatizo Moja

Uendeshaji wa ubatizo katika ulimwengu wa kikristo unatofautiana. Baadhi huzamisha, wengine hunyunyizia maji, bado wengine humiminia maji. Tabia ya umoja ambayo Roho huleta kwenye kanisa ni namna moja ya kufanya ubatizo (Efe.4:5). Ni nini maana ya ubatizo na umuhimu wake wa kiroho?

Maana ya Neno Ubatizo**.** Neno batiza linatokana na neno la kiingereza babtize ambalo linatokana na kigiriki baptizein. Kitenzi chake ni neno bapto ambalo lina maana ya kuzamisha majini. Matumizi ya neno ubatizo katika Agano Jipya humaanisha (1) ubatizo wa maji (Mt.3:6; Mk.1:9; Mdo. 2:41), (2) mfano wa kuteseka na kufa kwa Kristo (Mt.20:22, 23; Mk.10:38, 39; Luk.12:50) (3) ujio wa Roho Mtakatifu (Mt.3:11; Mk.1:8; Luk.3:16; Yoh.1:33; Mdo.1:5; 11:16) na (4) kutawadha au kuosha mikono (Mk.1:7:3, 4; Luk.11:38). Hakuna ushahidi wa kimaandiko kuwa ubatizo wa kunyunyiza ulitumika wakati wa mitume.

Ubatizo katika Agano Jipya. Matukio ya ubatizo katika Agano Jipya yalihusisha kuzamisha majini. Tunasoma kuwa Yohana alibatiza mto Yordani. (Mt.3:6; cf. Mk.1:5) na Ainon karibu na Salim kwa sababu kulikuwa na maji tele. (Yoh.3:23). Ni ubatizo wa kuzamisha ndio unaohitaji maji mengi. Yohana alimbatiza Yesu, Yordani (ndani) na baada ya kubatizwa Yesu alipanda kutoka majini (Mk.1:9, 10; cf Mt.3:16).

Kanisa la Mitume pia lilibatiza kwa kuzamisha majini. Wakati Mwinjilisti Filipo alipombatiza towashi wa Kushi, wote wawili walitelemka ndani ya maji na wote wawili walipanda kutoka majini baada ya ubatizo (Mdo.8:38, 39).

Ubatizo katika Historia. Hili ni somo linalojitegemea nje ya Biblia. Kidokezo ni kuwa Wayahudi walikuwa na tabia ya kuzamisha wafuasi. Pia iko michoro ya Waesene kule Qumram inayoonyesha ubatizo wa kuzamisha.

Maana ya Ubatizo

Maana ya ubatizo inahusiana na jinsi unavyofanyika. Ni baada tu ya mtu kubatizwa kwa kuzamishwa ndipo maana yake inapoonekana.

Ishara ya Kifo cha Yesu na Kufufuka. Kule kufunikwa na maji kunaashiria kugubikwa na masumbufu na mateso, (Zab.42:7; 69:2; 124:4, 5), hivyo ubatizo wa maji wa Yesu aliwakilisha onyesho la unabii la kuteseka, kifo na kuzikwa (Mk.10:38; Luk.12:50) na kuinuka

kwake kutoka kwenye maji kuliashiria kufufuka kwake kutoka wafu (Rum.6:3-5). Ubatizo ungekosa maana kitheolojia ikiwa Kanisa la Mitume lingetumia njia isiyo ya kuzamisha.

Ishara ya kuwa Mfu kwa dhambi na Kuwa Hai katika Kristo. Katika ubatizo, muumini huingia katika uzoefu wa kuteseka kwa Yesu. "Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima." (Rum.6:3, 4). Katika ubatizo, kifo cha Yesu kinakuwa kifo cha muumini na kufufuka kwa Yesu kunakuwa kufufuka kwa muumini.

1. Mfu kwa dhambi. Katika ubatizo waumini huwa "wameungana pamoja naye katika mfano wa mauti yake" (Kristo) (Rum.6:5) na kusulubiwa na Kristo (Gal.2:20). Hii inamaansiha utu wetu wa kale ulisu)lubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena. (Rum.6:6-8). Waumini wamekana mtindo wao wa zamani wa maisha, ya kale yanakuwa yamepita (2Kor.5:17), maisha yao yakiwa yamefichwa katika Kristo na katika Mungu. Ubatizo pia humaanisha kuzikwa na Kristo (Kol.2:12). Katika ubatizo, muumini huukana ulimwengu, kwa kutoka kati yake na kuishi maisha ya kutengwa na uchafu (2Kor.6:17). Kwenye Kanisa la Mitume, wito wa ubatizo pia uliita waumini kutubu. (Mdo.2:38). Hivyo, ubatizo ni utambulisho wa kutubu.

2. Kuwa Hai kwa Mungu. Uwezo ulio katika ufufuo wa Kristo hutenda kazi ndani yetu na kutufanya tutembee katika upya wa uzima. (Rum.6:4). Tunakuwa wafu kwa dhambi na tunakuwa hai kwa Mungu (Rum.6:11).

Ishara ya Uhusiano wa Kimaagano. Katika nyakati za Agano la Kale kutahiriwa kulikuwa ishara ya kimaagano baina ya Mungu na Ibrahimu. (Mwa.17:1-11). Agano la Ibrahimu lilibeba utambulisho wa kiroho na kitaifa pia. Kila mtoto aliyefikia umri wa siku nane na zaidi alipaswa kutahiriwa. (Mwa.17:10-14; 25-27). Mwanaume asiyetahiriwa alikatiliwa mbali (alitengwa) na watu wa Mungu kwa kuwa alikuwa amevunja agano. (Mwa.17:14). Desturi hii pia ilikuwa ishara ya kuhesabiwa haki kwa imani. (Rum.4:11). Peke yake haikutosha, bali kulidaiwa liwe jambo la moyoni. (Kumb.10:16; cf.30:6; Yer.4:4). Wasiotekeleza tohara ya moyoni wangeadhibiwa na mataifa. (Yer.9:25, 26).

Wayahudi walipomkataa Yesu kuwa Masihi, walivunja agano na Mungu, wakakoma kuwa wateule. (Dan.9;24-27, angalia somo la Mungu Mwana). Ijapokuwa agano la Mungu na ahadi zake zilibaki hizo hizo, alichagua watu wapya. Israeli wa kiroho walichukua nafasi ya Wayahudi. (Gal.3:27-29; 6:15, 16). Kifo cha Yesu kilihakikisha Agano Jipya, la kutahiriwa rohoni, kule kuitikia kwa imani kafara ya Kristo kwa njia ya kifo chake. (Gal.2:7). Agano Jipya linadai imani ya ndani siyo kitendo cha nje, kutahiriwa wala kutokutahiriwa siyo kitu, bali imani itendayo kazi kwa upendo (Gal.5:6; 6:15, 16). Kifo cha Yesu kiliridhia Agano Jipya. Watu huingia kwenye Agano hili kupitia tohara ya kiroho, imani kwa kifo cha Yesu kinalipia dhambi. Wakristo wana injili ya wasiotahiriwa (Gal.2:7). Mtu huingia kwa imani, utu wa ndani siyo kwa onyesho la nje. Hivyo kutahiriwa au kutokutahiriwa, hakufaidii kitu ila imani itendayo kazi katika upendo. (Gal.5:6). Kinachozingatiwa ni tohara ya moyo, katika Roho (Rum.2:28, 29). Ubatizo ni ishara ya kuingia mahusiano yanayookoa na Yesu (Kol.2:11, 12). Mwili wa dhambi huondoshwa kupitia tohara ya kiroho na muumini humvaa Yesu na kuingia mahusiano ya kimaagano na Yesu.

Wakiwa wa Kristo, wanakuwa uzao wa Ibrahimu, warithi wa ile ahadi. (Gal.3:27-29). Wanaoingia mahusiano ya namna hii wanapata uthibitisho wa Mungu kuwa "nitakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wangu" (Yer.31:33).

Ishara ya Kujitoa kwa Utumishi wa Kristo. Katika ubatizo wake, Yesu alijazwa Roho Mtakatifu. Hii ilikuwa ishara ya kutiwa mafuta kufanya utume aliopewa na Baba yake. (Mt.3:13-17; Mdo.10:38). Kwenye Kanisa la Mitume, kujazwa Roho Mtakatifu kulifuatia ubatizo wa maji. Hivyo nasi tunapobatizwa tunaungana na uwezo wa kimbingu na kwa na kutangaza injili. Roho Mtakatifu hutuandaa kwa utume. Yohana alisema ajaye "atabatiza kwa moto" (Mt.3:11). Isaya, alisema Mungu atatakasa watu wake "kwa roho ya hukumu na roho ya kuteketeza" (Isa.4:4), kuteketeza kabisa bati lako (Isa.1:25). Mungu ni moto ulao dhambi (Ebr.12:29). Akiisha kuzichoma dhambi, Roho hutoa karama. Kwenye Kanisa la Mitume, walijazwa ujasiri wa kuhubiri Neno. (Mdo.1:5, 8). Kwa siku za mwisho, kujazwa Roho kutakamilisha utume. (Mt.24:14; Ufu.14:6)

Ishara ya kuingia Kanisani. Ikiwa ishara ya mtu kuzaliwa mara ya pili (Yoh.3:3, 5), ubatizo hutia alama ya mtu kuingia kwenye ufalme wa Mungu. Wanafunzi waliongezeka kwa ubatizo (Mdo.2:41, 47; 1Kor.12:13). Hivyo, hakuna aliyebatizwa, akaacha kujiunga na familia ya kanisa.

Masharti ya kupewa Ubatizo

1. ***Imani.*** Imani inayotakiwa ni kukiri kuwa mauti ya Kristo ilimkomboa mwanadamu. (Mk.16:16). Ni wale tu waliomwamini Yesu ndio waliobatizwa hapo kale (Mdo.8:12, 36, 37; 18:8). Chanzo cha imani ni kusikia (Rum.10:17). Hivyo, kupeleka injili kwa kila kiumbe ni wito wa kuwa mwanafunzi hufanya mafundisho kuwa muhimu (Mt.28:19, 20)

2. ***Kutubu.*** "Tubuni mbatizwe", Petro alisema, (Mdo.238). Mafundisho ya Injili huleta pia toba na kuongoka.

3. ***Matunda ya toba.*** Wanaotaka ubatizo wapaswa kuonyesha matunda ya toba. (Mt.3;8). Matunda ya toba yatafanya wakae ndani ya Kristo na Kristo akae ndani yao. (Yoh.15:1-8).

4. ***Kupimwa.*** Kuwa mshiriki wa Kanisa ni huhusisha kuchukua hatua ya kiroho. Hivyo kupimwa ni muhimu ili kuwa na ushahidi wa kuonekana kuwa na imani, kutubu na kuwa na matunda ya toba kabla ya kukubaliwa kuingia kanisani.

***Je watoto wachanga nao wapaswa kubatizwa*?** Ubatizo huhusisha kuwaingiza kwenye ushirika wa kanisa waumini kwa mtazamo wa "kuzaliwa mara ya pili". Kuongoka kwao kunawastahilisha kubatizwa na kuwa washiriki wa Kanisa. Kufanywa washiriki wa kanisa hutokea kwenye kuzaliwa mara ya pili, siyo kwa kuzaliwa kimwili. Katika Agano Jipya wanaume na wanawake walibatizwa wakawa washiriki wa Kanisa. (Mdo.8:12, 13, 29-38; 9:17, 18; 1Kor.1:14). Hakuna popote katika Agano Jipya ambako ubatizo wa watoto wachanga unaruhusiwa au kuzuiwa. Kwa kuwa wachanga hawawezi kuongoka, hawana sifa ya kubatizwa. Yesu hakuwatenga watoto kwenye ufalme wake wa neema. "Waacheni watoto waje kwangu… walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao" (Mt.19:14, 15).

Kitendo cha Yesu kuwabariki watoto kumeingiza utaratibu wa kuwaweka wakfu watoto. Umri unaofaa kubatiza ni 1) Pale mtu anapokuwa anaweza kuelewa maana ya ubatizo 2) Wamejitoa kwa Yesu na kuongoka 3)Wanaelewa misingi ya ukristo 4) Wanafahamu umuhimu wa kuwa mshiriki wa kanisa. Mtu huhatarisha wokovu wake anapokuwa amefikia umri wa kuwajibika na kukataa mvuto wa Roho Mtakatifu. Wazazi wanaokubali watoto wao wabatizwe wakiwa wadogo, ni lazima wakubali jukumu la kuwalea wapate kukua kiroho na kukuza tabia njema. Kwa kuwa kukomaa hutofautiana, hakuna umri uliowekwa kwa ajili ya mtu kubatizwa.

Matunda ya Ubatizo

Tunda maarufu la ubatizo ni kumwishia Kristo. Malengo na matamanio humlenga Kristo siyo nafsi. “Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko… Kwa maana mlikufa na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. (Kol.3:1-3). Ubatizo siyo upeo bali tunapompokea Yesu, tunaingia katika mpango wa Mungu wa kukua. “Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu.” (2Pet.1:2).

Tunda la pili ni maisha ya kuishi kwa ajili ya Kanisa la Kristo. Hatuwi tena watu waliotengana bali tunakuwa mawe yanayojenga hekalu la Mungu (2Pet.2:2-5).Tunaingia kwenye mahusiano maalum ambayo hutufanya tupokee daima neema ya Mungu inayotuwezesha kukua katika upendo. (Efe.4:16). Tunachukua majukumu miongoni mwa wenye maagano na Mungu kulea waumini wapya (1Kor12:12-26). Kwa ustawi wao na wa kanisa, waumini wapya wapaswa kujihusisha na maisha ya ibada na huduma ya upendo. (Efe.4:16).

Tunda la mwisho ni maisha ya kuishi kwa ajili ya ulimwengu. Ni kweli baada ya kubatizwa wenyeji wetu ni mbinguni (Wafilp 3:20). Hata hivyo tumeitwa tutoke ulimwengu na kufundishwa kushiriki huduma ya Yesu ya kuokoa. “Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.” (Mdo.22:16).